



Basi Jua, rehma ya Allaah iwe juu yako, kwamba ni **wajib** (lazima) juu yako kujuwa mambo **mane**:

- (1) (Al il'm) La kwanza ni **ilimu** , ambayo ni ma'arifa ya Allaah na ma'arifa ya Nabii (Mtume) na ma'arifa ya dini ya Kislamu kwa dalili .
- (2) La pili ni **kutenda amali** kutokana na hii Ma'arifa.
- (3) La tatu ni **kuita watu** kwenye njia hii.
- (4) La nne ni **kuwa na Subira** kwenye njia hii.

Na dalili yake ni kauli ya Allaah (taa'la): (kama ilivyofasiriwa)

وَالْعَصْرِ ①
إِنَّ الْإِنْسَانَ لَفِي خُسْرٍ ②
إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَّصُوا بِالحَقِّ وَتَوَّصُوا بِالصَّبْرِ ③

Naapa kwa Zama! Hakika binaadamu bila ya shaka yumo katika khasara, ila wale walio amini, na wakatenda mema, na wakahusiana kwa haki, na wakahusiana kusubiri. (Soorat al-Asr 103)

Imam Shafi'ee (rehma ya Allaah iwe juu yake) alisema: Ingekua Allaah ameshukisha Surah hii peke kama Hoja juu ya maumbile yake ingekuwa ime watosheleza.

Imam Bukhaaree (rehma ya Allaah iwe juu yake) alisema katika Mlango: **Elimu kabla ya Kauli na Amali** ' na dalili ni kauli ya Allaah (Subhanahu wataa'la)

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

Basi jua ya kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa ila Allaah (Soorah Muhammad 47:19)

Hivyo basi ali anza kwa kutaja Elimu kabla ya Kauli na Amali.

Jua basi, Rehma ya Allaah iwe juu yako, kwamba ni **wajib** (lazima) juu ya kila muislamu mwanamume na mwanamke kujifunza na kutenda amali juu ya mambo haya **matatu** .

La Kwanza: ni kujua kwamba ni Allaah ndiye aliye Tuumba na kutupa Rizki sisi sote na wala na hakufanya hivyo bila ya sababu yeyote. Bali ametutumiya rasool (Mtume), na yoyote anaye mtii (fuata) ataingiya peponi, na anaye muasi (halifu) ata ingiya motoni: na dalili ni kauli ya Allaah (ta'la): (kama ilivyofasiriwa)

إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَا أَرْسَلْنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ
رَسُولًا ﴿١٥﴾ فَعَصَىٰ فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ فَأَخَذْنَاهُ أَخْذًا وَبِيلاً ﴿١٦﴾

Hakika Sisi tumemtuma kwenu Mtume aliye shahidi juu yenu, kama tulivyo mtuma Mtume kwa Firauni. Lakini Firauni alimuasi huyo Mtume, basi tukamshika mshiko wa mateso. (Soorah al-Muzammil 73:15-16)

La Pili ni kujua ya kwamba Allaah haridhiki mtu yoyote ashirikisishwe na yeye kwenye Ibadah, hata iwe malaika aliyuko karibu (mfano Jibril) , wala mja aliye tumwa (mfano Mtume Muhammad ﷺ). Na dalili ni kauli ya Allaah (Subhanahu wata'la) (kama ilivyo fasiriwa):

وَأَنَّ الْمَسَاجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا

Na hakika misikiti ni ya Allaah, basi musimombe (yani msimuabudu) yeyote pamoja na Allaah . (Soorah al-Jinn 72:18)

La tatu yoyote anaye mtii (mfuata) Mtume na akamuabudu Allaah bila ya kumshirikisha, basi haijuzu kwa mtu huyo kufanya urafiki na mapatano na wale wanaompinga Allaah na Mtume wake, hata kama ni watu walioko karibu naye, na dalili ni kauli ya Allaah (kama ilivyofasiriwa):

لَا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ
وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ أُولَئِكَ كَتَبَ
فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ
تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ أُولَئِكَ
حِزْبُ اللَّهِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٢٢﴾

Huwakuti watu wanao muamini Allaah na Siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wanao mpinga Allaah na Mtume wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao. Hao ameandika katika nyoyo zao Imani, na amewapa nguvu kwa Roho itokayo kwake. Na atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito kati yake. Humo watakaa daima. Allaah yuko radhi nao, na wao wako radhi naye. Hao ndio Hizbullahi, (Kundi la Allaah). Hakika Kundi la Allaah ndilo lenye kufanikiwa. (Soorah al-Mujaadilah 58:22)

Basi Jua, Akuongoze Allaah kwenye kumtii amri zake, njia ya haki na iliyo nyoka ni ya Ibrahim nikumuabudu Allaah bila ya kumshirikisha kwa kumtakasia Dini. Hii ndiyo amrisha la Allaah kwa watu wote na ni kwa sababu hii amewaumba kama alivyosema Allaah (ta'ala)

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi (Soorah adh-Dhaariyat 51:56).

Na maana ya waniabudu mimi (ibaadah) hapa ni kumtakasia Allaah ibadah peke. Jambo muhimu kabisa aliyo amrisha na Allaah ni Tawheed na nikuambudu Allaah bila ya kumshirikisha na chochote. Jambo ovu kabisa aliyo likatiza Allaah ni Shirki, na nikuawaomba wengine pembeni ya Allaah (maana kuabudu kitu ama mtu yoyote mwingine) na dalili ni kauli ya Allaah (ta'ala)

وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا^ط

Muabuduni Allaah wala msimshirikishe na chochote (Soorah An-Nisa' 4:36)

Basi ukiulizwa: ni vitu gani vitatu katika usooli ya dini ambavyo ni wajibu kuwa na ma'arifa navyo (kuvijuwa), Basi sema ni kwa mja kuwa na maa'rifa Ya Mola wake (Allaah), na dini yake (Islaam), na ya Mtume wake Muhammad ﷺ.